**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**684** **VITENDO VYA KUJIFUNZA SANAA**

**Muda: Saa 3.** **Year: 2006**

---

**Maelekezo.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A**, **B** na **C.**
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu **A** na maswali **mawili (2)** kutoka katika kila sehemu **B** na **C.**
3. Andika majibu yako kwa kalamu ya wino wa bluu au mweusi isipokuwa michoro ambayo itachorwa kwa penseli.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Taja ala nne za muziki ambazo zikipigwa hutoa sauti yenye urefu mfupi sana.
2. Eleza mbinu tatu za kuunda udongo zinazofaa kwa mikono midogo ya watoto.
3. Fafanua umuhimu wa kufundisha dhana ya nafasi katika uchoraji kwa watoto wa Elimu ya Awali.
4. Bainisha faida nne za mwalimu kuandaa kitabu cha kazi za sanaa za kila mtoto.
5. Taja jinsi unavyoweza kutumia rangi za msingi kutengeneza rangi ya kijani.
6. Eleza tofauti tatu kati ya sanaa za jukwaa na sanaa za ufundi.
7. Orodhesha vifaa vinne vinavyoweza kutumiwa kama kibadala cha udongo katika ufinyanzi.
8. Taja sifa nne za sauti ya mtoto katika kuimba.
9. Bainisha matumizi manne ya **soga** kwa watoto wa Elimu ya Awali.
10. Kwa kifup, eleza maana ya dhana zifuatazo kama zinavyotumika katika ufundishaji naujifunzaji wa Watoto wa elimu ya Awali:

    (a) Mbinu

    (b) Zana

## SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali mawili (2) kutoka katika sehemu hii.

11. Orodhesha aina tatu za michezo ya kuigiza inayoweza kutumiwa kama tiba kwa watoto wenye changamoto za kihisia. Kisha fafanua umuhimu wake kwa kila aina.
12. Changanua faida tano za ufinyanzi wa bure kwa ukuaji wa mtoto wa Elimu ya Awali.
13. Kwa kutoa hoja tano eleza kwa nini vifaa chakavu ni muhimu sana katika masomo ya uundaji.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU C (Alama 30)**

Jibu maswali mawili (2) kutoka katika sehemu hii.

14. Fafanua mbinu sita za ufundishaji wa Vitendo vya Kujifunza Sanaa zinazompa mtoto nafasi kubwa ya ushiriki.
15. Eleza umuhimu wa kufanya tathmini endelevu katika somo la Vitendo vya Kujifunza Sanaa. Toa hoja sita.
16. Changanua vigezo vitano vya kuzingatia wakati wa kuchagua vifaa vya uchoraji kwa ajili ya watoto wa Elimu ya Awali.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org